# Ukamilifu na Utimilifu wa Kifasihi katika Maandishi ya Kubuni: Mfano wa Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed

*Jackson Mutuku Kavoi*
*Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Tanzania*

**Ikisiri**

**Makala haya yanalenga kuhakiki muwala au mshikamano wa viambajengo vya fani katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed: *Dunia Mti Mkavu* (1980) na *Kiza Katika Nuru* (1988). Uhakiki huu unahusisha viambajengo vinne tu vya fani: wahusika, msuko, mandhari na mtindo. Lengo kuu la uhakiki huu ni kuonyesha ni kwa vipi muwala au muumano wa vipengele vya fani unachangia kudhihirisha ukamilifu na utimilifu wa kifasihi katika kazi ya sanaa kupitia riwaya hizi. Kwa kufanya hivyo, mhakiki anachunguza iwapo riwaya hizi zinadhihirisha muwala wa vipengele vya msuko, usawiri wa wahusika, mandhari na mtindo, hivyo kumwezesha kufikia maamuzi iwapo riwaya husika zimefikia ukamilifu na utimilifu wa kifasihi. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa ili kazi ya ubunaji idhihirishe ukamilifu na utimilifu wa kifasihi, ni sharti viambajengo vya fani vidhihirishe muwala au muumano. Katika mkabala huu, makala hii inadadavua jinsi riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* (1980) inavyokosa muwala ikilinganishwa na riwaya ya *Kiza Katika Nuru* (1988), hivyo umaarufu wake kutopata uhai kifani kwa kiasi fulani, tofauti na vile Mazrui (1984) anavyogundua kwa upande wa maudhui. Halikadhalika, matokeo ya uhakiki huu yamedhihirisha kuwa, mpangilio dhoofu wa matukio kiwakati, unaathiri uumbaji wa wahusika na msuko wa matukio katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* (1980) hali inayoinyima ukamilifu na utimilifu wa kifasihi kwa kiwango fulani, tofauti na riwaya ya *Kiza Katika Nuru* (1988).**

**Maneno Muhimu**: Muwala, Ukamilifu, Utimilifu, Viambajengo, Fani, Maandishi ya Kubuni

## Utangulizi

Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza jinsi viambajengo vya fani vinavyodhihirisha muwala au muumano katika riwaya za Said Ahmed Mohamed: *Dunia Mti Mkavu (1980)* na *Kiza Katika Nuru (1988)*, huku mhakiki akitaka kutathmini kama riwaya husika zimefikia ukamilifu na utimilifu wa kifasihi. Mhakiki katika kuteua *Dunia Mti Mkavu* ameongozwa na maoni ya Mazrui (1984) kuwa hii ndiyo riwaya ya S. A. Mohamed iliyo bora kwa upande wa maudhui. Kwa hivyo, makala haya yanataka kuchunguza iwapo sifa ambazo

riwaya hii imepata kwa upande wa maudhui zinaweza kuwepo katika fani au la. Vivyo hivyo, *Kiza Katika Nuru* imeteuliwa kinasibu. Kwa ujumla, riwaya zake nyingine ni *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Tata za Asumini* (1990), *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006), *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Mkama Dume* (2012), *Mhanga Nafsi Yangu* (2013), *Kamwe si Mbali Tena* (2014). Kando na riwaya, pia ameandika kazi za kishairi: *'Sikate Tamaa* (1980), *Kina cha Maisha* (1984) na upande wa tamthilia ameandika *Pungwa* (1988), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Amezidi* (1995). Pia, ameandika kazi za kinadharia na fasihi simulizi (Jessee, Wafula na King'ei, 2018). Aidha, mwandishi wa makala haya anataka kuweka wazi kuwa, hazingatii viambajengo vyote vya fani bali anazingatia wahusika, msuko, mandhari na mtindo. Kwa kuzingatia vipengele hivi, anaongozwa na imani kuwa, anakuwa katika nafasi nzuri ya kukadiria muwala wa vipengele hivi katika riwaya anazozihakiki kikamilifu. Vilevile, vipengele hivi ndivyo mihimili mikuu ya kazi yoyote ya ubunifu (Kimmey, 1976).

Mwandishi wa makala haya anaongozwa na mtazamo wa nadharia ya Umuundo ili kushughulikia fani katika riwaya teule za Said Ahmed Mohamed kikamilifu. Katika makala hii, Umuundo unachukuliwa kama "mtazamo wenye kuzingatia ujumla wa vitu na mahusiano ya vitu hivyo katika kujenga kitu kimoja" (Scholes, 1974, uk.2). Waaidha, uhakiki huu hahujihusishi na wanaumuundo wote, bali unajikita hasa na wanaumuundo waliozingatia Umuundo katika kuhakiki kazi za fasihi. Kwa mkabala huu, Barthes (1966) ana maoni kuwa, wanaisimu wanachunguza sentensi na kutazama jinsi ambavyo maneno mbalimbali yanaunganishwa na kuiunda na kuipa maana. Vivyo hivyo, badala ya kujikita katika kiwango cha sentensi, huchunguza hadithi kwa kuangalia sehemu mbalimbali zinavyoiunda na kuipatia maana. Kwa mujibu wa Barthes (1966), mwandishi wa makala haya anachukulia kuwa, riwaya ina sehemu tofauti zinazojengana, kama ilivyo katika hadithi. Sehemu hizi ni wahusika, msuko, mandhari na mtindo. Hivyo basi, makala hii inazingatia riwaya teule za Said Ahmed Mohamed, huku ikisisitiza uhusiano wa vipengele hivi kulingana na jinsi wanaumuundo wanavyoiangalia sentensi kama kitu kinzima.

## Dhana ya Muwala

Katika uhakiki huu, dhana ya muwala inachukuliwa kama mshikamano au muumano wa vipengele vya fani katika kukamilisha muundo wa riwaya nzima. Mtunzi wa kazi ya sanaa anapoanza safari ndefu ya uandishi, huongozwa na vigezo fulani kwa hali kwamba hupanga matukio ya kazi yake akitarajia yaende sambamba na matendo ya wahusika, mazingira anayowajengea na, vilevile, lugha anayowamilikisha. Mtizamo huu wa Friye (1957) ni muhimu katika kumuongoza mtunzi kujenga riwaya, tamthilia au hadithi fupi yenye vipengele vinavyoumana na kuoana ili kukamilisha kazi ya ubunifu (kama inavyonukuliwa katika

Eagleton, 1983, uk.93). Vipengele vya fani ndio malighafi ya watunzi wa maandishi ya kubuni tofauti na wachongaji wa sanamu ambao wanahitaji miti. Kulingana na wanaumuundo, ikiwa mtunzi wa kazi ya ubunifu anajenga vipengele ambavyo vinapinga kanuni za muwala, basi utunzi wake utakuwa haujafaulu chambilecho Newton (1988:45) kuwa:

> Umuhimu wa uhakiki ... ni kuchunguza jinsi umoja wa kazi ya ubunifu inavyofaulu au kutofaulu na uhusiano wa vipengele tofauti vinavyoendelea kujenga umoja huu.

Kulingana na Newton (1988), iwapo vipengele vinavyoiumba kazi ya ubunifu vinaonyesha hali ya kutoumana, basi, kazi hiyo haikosi kutangazwa kuwa na doa, hivyo basi, kutofikia ukamilifu na utimilifu wa kifasihi. Ingawa riwaya imejengwa kwa vipengele tofautitofauti, haiba yake inategemea muwala na mahusiano ya vipengele husika ili kuleta maana timilifu. Kwa mkabala huu, ni vigumu kutoa kauli mwafaka, na isiyo na mushkeli kuhusu urembo wake kwa kuchunguza kipengele kimoja tu bila kukihusisha na vile vingine. Levi-Strauss (1967: 207), akigusia mahusiano ya visehemu tofauti vya visaasili, anasisitiza kuwa:

> Maumbo halisi ya vipengele vya kisaasili sio mahusiano yaliyojitenga, bali ni mirundo ya mahusiano hayo, na ni katika mirundo hii tu ambapo mahusiano haya yanaweza kutumika na kuunganishwa ili yaweze kutoa maana.

Ijapokuwa Levi-Strauss (1967) anazungumzia sehemu moja ya Fasihi Simulizi – visaasili, tunaweza kutumia maoni yake katika uchambuzi wa riwaya. Hivyo, kulingana na maoni yake, makala haya yanajishughulisha kwa kuchunguza mahusiano hakikiwa bila kuvitenganisha; jambo ambalo linamwezesha mhakiki wa riwaya hakikiwa kukadiria ukamilifu na utimilifu wake kwa kuzingatia kigezo cha muwala.

## Muwala wa msuko, wahusika, mandhari na mtindo katika *Dunia Mti Mkavu* (1980)

Msuko wa *Dunia Mti Mkavu* (1980) una misingi yake katika msuguano wa kitabaka baina ya wala kuku na wala kama kuku (wenye navyo na wasio navyo). Migogoro yote inayoisukuma mbele msuko wa riwaya hii ni zao la kitabaka kama inavyojitokeza katika riwaya yake nyingine— A*sali Chungu* (1977). Msuguano huu ni baina ya tabaka la wala kuku (mabwanyenye na wakoloni) na wala kama kuku (mafalahi, makuli, wafanyakazi wa viwandani na wazururaji). Msanii ameazimia matukio yote ya riwaya hii yanatendeka kati ya mashambani na mjini. Mandhari anayoyachora na kuwajengea wahusika wake yanaenda sambamba na hulka zao (wahusika wake). Hivyo, makazi ya wachochole yanachangia katika kuleta maana ya hali zao za ufakiri, huku mandhari ya waliotukuka kama

mabwanyenye yakifafanua ukwasi wao. Hatuhitaji kuelezewa zaidi kibanda cha Fumu ambacho kimerembwa na "kitanda cha kamba chenye tendegu moja lililoteguka, kiti cha marimba, jembe lililolika bapa, mndu na kibuyu cha maji kilichoning'inia ukutani" (uk.3). Fauka ya ulitima huu wa kimali, pia, kuna ufakiri wa afya. Tunaelezewa kuwa donda ndugu lililokuwa mguuni mwa Fumu lilikuwa limemhangaisha kwa muda mrefu (uk.1).

Halikadhalika, chumba cha Bakari sio tofauti kwani kinavikwa taji na sanduku la msonobari, huku likisheheni mararu ya shati. Vivyo hivyo, mandhari anayomchorea Pandu na Staghafiru, mamake wa kupanga, hayatofautiani kamwe na ya ndugu zake. Chumba anacholala Staghafiru ni ishara ya unobe uliosakini miongoni mwa wachochole. Mazingira haya, bila kubakisha, yanadhihirisha sura ya fukara na ufakiri wake. Kuanzia mwanzo hadi hatima ya riwaya, tunagundua mandhari yanayokinzana; mazingira ya unobe yakikinzana na ya kikwasi. Mkinzano huu haukosi kuonekana tunapopiga darubini chumba cha Inspekta Farouk, kwa jina lingine Kibwana, na wazee wake Bi. Nafisa na Hilal. Chumba chake kinachorwa hivi: "shiti nyeupe lililonyooka kwenye vitanda viwili vya vono, futi nnenne, vinavyounganishwa; na mito yake miwili, mmoja pembe hii na mmoja pembe nyingine" (uk.77). Mapambo ya chumba hiki hayaishi kwani zaidi kuna kabati kubwa kuekea nguo, "*dressing table*".

Bila shaka, mandhari haya yanadhihirisha tofauti iliyopo baina ya matabaka mbalimbali yaliyokuwa yakiishi Unguja wakati huo. Yote yanawachochea wahusika wanaowakilisha tabaka nyanyaswa kihisia, huku yakiwashajiisha waitikie kama inavyotarajiwa. Yanawafanya kujiuliza kwa nini, kwa vipi na kwa sababu gani. Tunamwona Fumu, baada ya kukagua chumba chake anapoamka, anajiuliza maswali haya (uk.4). Vivyo hivyo, yanamwathiri Bakari hadi kufikia uamuzi kuwa pesa ndio kitovu cha maovu yote yanayoikumba jamii yake. Kwa mkabala huu, hatukosei tunapotoa kauli kuwa mandhari ambayo mtunzi anawajengea wahusika wake yana muumano na matendo yao, yanayohusiana kikamilifu kwani yanawahamasisha kuitikia inapohitajika, hivyo kutufanya tuone mabadiliko ya tabia zao. Kimmey (1976: 147), akigusia uhusiano uliopo baina ya mandhari na wahusika anasisitiza kuwa:

> ... mandhari haitumiki tu kuremba mazingira ya hadithi, lakini pia husaidia kukuza muundo na **huathiri wahusika**. (*Msisitizo ni wa mwandishi wa makala hii.*)

Kulingana na Kimmey, licha ya mandhari kutumika kutia heba ya hadithi, pia, yanasaidia kuathiri wahusika. Kimmey (1976) anapotaja kuathirika kwa wahusika na mandhari anamaanisha kuwachochea na kuwashajiisha kitabia kama inavyojitokeza kwa Fumu, Bakari na Pandu. Vivyo hivyo, hatuchelewi kuona jinsi mandhari yanayomzunguka Inspekta Farouk yanamwathiri; hivyo, kujiona mtu aliyetukuka na kufanikiwa katika maisha yake. Hii ndio sababu

anapotaarifiwa na mamake mlezi kuwa Suleiman alikuwa amekubali kumuoa Lulua, bintiye, anatoa kauli hii: "Ala umeshamtoka ujinga wake, ... kwa nini bibiye hamkumfahamisha vilivyo; mimi ni mweusi ngozi tu damu yangu ina nasaba nyeupe; au hafahamu?" Bila shaka, hatukosi kukiona kiburi cha Farouk kupitia usemi huu. Tukio la Suleiman kumkataza Farouk kumuoa bintiye Lulua, ni ishara ya ubaguzi wa rangi uliokuwa umesakini kisiwani Unguja.

Mandhari yanapotoa ufafanuzi wa hulka za wahusika, wakati huohuo, yanachangia katika kuendeleza na kukuza msuko wa riwaya husika. Mandhari katika *Dunia Mti Mkavu* yanafuma matukio mbalimbali na kuyaunganisha kiasi kwamba matukio husika yanaumana kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mandhari anayomchorea Fumu, huku makazi yake yakionekana ya kusikitisha, yanamfanya kujiuliza kwa nini mateso haya yatukie. Ni kutokana na ushawishi huu wa kimandhari ambapo Fumu yuko tayari kupambana na Fauz ingawa ana mndu hali mwenzake ana bunduki. Fumu hawezi kustahimili zaidi ujeuri wa Fauz. Kwa hali hii, mgogoro mkubwa baina ya mafahali hawa unatokana na yale yanayowazingira. Migogoro hii inaisukuma mbele msuko wa matukio hadi kuufikisha kileleni– mgomo. Vivyo hivyo, makazi anayomjengea Bakari na makuli wenzake, huku yakitishia hatari, inawahamasisha kuchukua silaha na kupambana na wanyonyaji wa nguvu zao. Hivyo, ni wazi kuwa mandhari ambayo mwandishi anawajengea wahusika wake yanashirikiana, moja kwa moja, kukuza msuko wa riwaya hii. Ili kutilia mihimili suala hili Kimmey (1976) anasema:

> Mandhari ... huunganisha msuko na wakati maalum na mahali, hufafanua wahusika na maana ya kile kinachotukia ... mandhari ... hutekeleza sehemu muhimu katika kuwasilisha msuko mzima.

Aanachokifafanua Kimmey ni kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya msuko na mandhari kiasi kwamba, mandhari husaidia kutoa maana ya hadithi nzima na huwasilisha msuko. Waaidha, anasisitiza zaidi kuwa mandhari hufunua hulka za wahusika. Maoni ya Kimmey si pweke kwani Warren (1961), akisisitiza muumano wa viambajengo vya fani anasema kuwa "uhakiki wa riwaya kwa kawaida umeainisha vipengele muhimu: msuko, uhusika na mandhari ..." (uk.196). Maoni ya Warren (1961) yanaoana na ya Kimmey (1976) kwa hali kwamba, vipengele hivi vyote hufanya kazi kwa pamoja katika maandishi ya kubuni, na hasa, kwa muktadha huu, riwaya.

Mbali na haya, muwala wa msuko na uumbaji wa wahusika ni viungo muhimu katika ujenzi wa riwaya au kazi yoyote ya ubunifu. Hii ni kwa sababu migogoro ya wahusika husukuma msuko mbele. Bila migogoro, haiwezi kusonga mbele. Mgogoro unaodhihirika zaidi, na ambao unaupeleka msuko wa *Dunia Mti Mkavu* mbele, ni baina ya mhusika mmoja na mwingine. Tunashuhudia mgogoro wa Fauz na Fumu ambao una misingi yake katika mahusiano ya Fumu na Masika. Huu ni mgogoro wa kitabaka ambao unadhihirisha uhusiano uliopo baina ya

mabwanyenye na mafalahi. Matukio yanayoandamana na mgogoro huu yanamsaidia mwandishi kumsawiri Fauz, huku akionyesha utukufu, utausi na ukatili wa mabwanyenye kwa ujumla. Pia, unatuwasilishia Fauz akiwa amesawiriwa kama kielelezo cha mabwanyenye wote. Mchuano baina ya Bakari na Mbwana ni dhihirisho ya tabia sugu ya vibaraka waliokuwa wakisaidiana na wakoloni kuwanyanyasa makuli. Kupitia mgogoro huu, tunafahamu hasira za Bakari ambazo zinafanana na za Fumu ambaye yu tayari kumuangamiza Fauz anapochoma mahindi yake.

Moja kwa moja, muwala na uhusiano uliopo baina ya wahusika na msuko wa *Dunia Mti Mkavu* unadhihirika Mohamed anapojenga msuko wa riwaya hii, huku akitumia matabaka mbalimbali ambayo matendo yao na matamanio yao yanaenda sambamba na matabaka wanayoyawakilisha. Kwa kiasi kikubwa migogoro inayotukia baina ya wahusika, hivyo kuendeleza msuko, ina mizizi yake katika matabaka yote matatu (mafalahi, makuli na wazururaji) yanayotaka kujinasua kutoka unyanyasaji wa tabaka linalomiliki nyenzo za uchumi.

Tunapochunguza zaidi riwaya hii kimtindo, tunafahamu jinsi mbinu rejeshi inavyosaidia kuunga matukio mbalimbali kwa pamoja. Kwa kutumia mbinu hii, mtunzi anaepukana na kile Ngara (1982) anachokiita “muundo wa kimwandamano” (uk.15) ambao unamfanya msomaji kufuata matukio bila kufikiria. Kwa muktadha huu, muundo wa kimwandamano una maana ya msuko sahili ambao matukio yake yanafuatana moja kwa moja.

Said Ahmed Mohamed anatumia mbinu rejeshi kwa ufundi mkubwa, huku akifuma kwa pamoja matukio mbalimbali katika msuko mzima. Mathalani, hatujui ni kwa nini Jaku anatiwa ndani hadi kupitia mbinu rejeshi ikifungamana na uzungumzi nafsia wa Farouk na Jaku mwenyewe. Pia, kwa kuwaingia wahusika wake akilini, tabia za wahusika wengine zinaeleweka. Halikadhalika, busara za Mzee Gae kupitia uzungumzi nafsia wa Pandu ambao unajitokeza kwa namna ya mbinu rejeshi. Aidha, inafahamika ni kwa nini matukio katika msuko wa riwaya hii yatukie. Pia, tabia ya baadhi ya wahusika, hususan Mzee Kumba na Mzee Gae ambao wanajitokeza kama wazee wenye busara zinafahamika. Mzee Jaku, anayesawiriwa kama mhusika asiye na akili na katili, tabia zake zinaeleweka kupitia uzungumzi nafsia wa Bipole anapokadiria yaliyompata (uk.73). Pia, hatukosi kuona ujeuri na utausi wa Farouk anapokadiria alivyomtia Mzee Jaku mbaroni na hatimaye kusababisha kifungo chake.

Zaidi ya haya, tunapokadiria jazanda anazotumia, zinavyochangia katika kufunua tabia za wahusika na ujenzi wa mandhari. Mzee Gae anapojifananisha na simba hali Fumu na maiti. Tunaumba akilini mwetu ukali wa simba na kutojiweza kwa maiti. Hivyo, hulka zao zinadhihirika moja kwa moja. Aidha, mandhari anayoyachora ya msonobari (uk. 24) yanafafanua uthabiti wa mabwanyenye. Hii ndio sababu “alishusha pumzi, akajiambia kimoyomoyo,

‘mkono mmoja hauwezi kuutikiza mti huu” (uk. 25). Kupitia jazanda ya msonobari, mandhari ya uthabiti wa mabwanyenye na wakoloni yanadhihirika–walikuwa na nguvu nyingi kiasi kwamba mwananchi mmoja kama Fumu hangeweza kufanya lolote bila kuomba usaidizi wa wananchi wengine. Licha ya haya, kupitia jazanda hii tunashuhudia muungano wa wananchi ili waweze kuung’oa msonobari (mabwanyenye na wakoloni) unahitajika. Kufikia hapa, bila shaka, jazanda hii ambayo ni kipengee muhimu cha mtindo inaonyesha, bila kubakisha, ufungamano uliopo miongoni mwa msuko, mandhari, usawiri wa wahusika na mtindo.

Ingawa kuna muwala wa mandhari, wahusika na mbinu za kimtindo katika riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, muwala huu unakosekana baina ya msuko na uumbaji wa wahusika na mpangilio wa matukio kiwakati unapochunguzwa. Baadhi ya matukio kiwakati yapoangaliwa kwa jicho la upekuzi, hayakubaliki kamwe. Hayafungamani kabisa na wahusika, jambo ambalo linadhoofisha muwala wa riwaya hii kimuundo. Kwa mfano, tukio la Jaku kuhukumiwa jela na mtoto wake Kibwana, tunapolihakiki kwa makini halikubaliki kiwakati. Kisa na maana ni kuwa, Kibwana alizaliwa pacha na Bakari (uk. 72), na wakati mama yao alipofariki Bakari alikuwa na umri wa miaka mitano (uk. 40), na alilelewa na Bi. Mboje. Hata Bipole anaonekana kupitia uzungumzi nafsia akisononeka kwa sababu ya kupokonywa mtoto wake, Kibwana. Vilevile, ni wakati huo anapodokeza kwamba Jaku, mumewe, kafungwa miaka kumi na mitano (uk. 74). Swali ni kwamba, aliyemfanyia Mzee Jaku mashtaka ni aliyepaswa kuwa mwanaye Kibwana (Inspekta Farouk) akiwa na umri wa miaka mitano kama Bakari waliokuwa mapacha au ni Kibwana mwingine? Matukio haya kiwakati hayaingii akilini kamwe hali ambayo inaudhoofisha muwala wa msuko wa riwaya hii pamoja na wahusika wake, hivyo kutia tashwishi anayotuwasilishia mtunzi.

Ukosefu wa muwala na uhusiano wa matukio na wahusika haukomei hapa, kwani inadhihirika Masika akiozwa kwa nguvu na Makame, babaake, kwa Fauz, huku akishirikiana na Hamoud, babaake Fauz (uk. 21). Kulingana na maelezo ya mtunzi, Hamoud ndiye anapaswa kuwa aliuliwa na Mzee Jaku wakati Fauz alipokuwa mtoto mdogo. Haya yote yanajitokeza katika maelezo ya mwandishi anapokadiria yanayompata Mzee Jaku awali baada ya kuachiliwa kutoka jela. Anasema:

> Alijaribu [Jaku] kukumbuka yaliyopita. Aliivuta ile siku aliyokuwa akinoa mndu wake kwa tupa, akamwona Bakari, mwanawe, akimjia damu zinamchiririka usoni, amechorwa kisu na Fauz, mtoto wa Bwana Hamoud ... Safari hii Jaku aliona vi mno. Alitoka na mndu wake, akamkuta Hamoud naye amesimama na bunduki yake. Jaku hakusita; lakini mama Jaku, Bipole alikwenda kumzuia mumewe ... Hilo ndilo alilolikumbuka kulifanya na wala si jingine. Aliposikia Bwana Hamoud

> amechinjwa ... na yeye anatafutwa na polisi. Na huo ukawa mwanzo wa kisirani kilichomfungisha bure kifungo kirefu (uk. 117).

Dondoo hii inapoambatanishwa na matukio ya awali, ni wazi Fauz na Masika waliozwa baada ya kifo cha Bwana Hamoud. Fauz alikuwa marika na Bakari ambaye alizaliwa pacha na Kibwana, na aliyemfingisha babake kama inspekta wa polisi. Vilevile, mama yao alikufa Bakari akiwa na umri wa miaka mitano, na ni wakati huu ambapo Hamoud aliuliwa. Hivyo, inafuata kuwa Fauz hangeoa akiwa na umri wa miaka mitano. Ni wazi kuwa kipengele hiki cha upangaji wa matukio kiwakati, kinapofungamanishwa na cha wahusika, kinaudhoofisha muwala wa msuko wa riwaya hii. Kusema kweli, kama wasomaji, hatuwezi kusema au kutambua tukio lililotukia mwanzo kukiwa na tashwishi kuhusiana na umri wa wahusika. Kuhusu swala hili Perrine (1978: 64) analifafanua hivi:

> Matukio yanahitajika kupangwa kwa njia inayofaa, ambayo si lazima yatiririke moja kwa moja, lakini yanapopangwa tena, sharti yafuate mwendelezo wa kimantiki. Katika hadithi iliyo na mshikamano, kila tukio hukua kutoka tukio tangulizi kiwakati na huendelea katika muwala na usababishano na muathiriano.

Mwendelezo huu wa kimantiki na ukuaji wa matukio kiwakati unakosekana katika msuko wa riwaya hii, jambo ambalo linaipokonya umaarufu wake kwa kiasi fulani. Upangaji wa matukio kiwakati unaoipokonya riwaya hii muwala wake kiasi kwamba, baadhi ya matukio hayaaminiki. Tukio la Masika akiwa amefungwa pingu kuwapokonya askari wawili bunduki na kumchoma Inspekta Farouk kwa singe hayasawiriki. Kama angekuwa amefunguliwa pingu tungeamini yale mwandishi anayotaka tuyaamini. Tukio hili haliendi sambamba na uwezo wa Masika mwenyewe. Kwa vyovyote vile, James (1961) hakosei anapouliza "mhusika ni nini isipokuwa kisababisho cha tukio? Tukio ni nini isipokuwa ufunuzi wa mhusika?" (uk.302). Kulingana na maoni ya James, matendo ya Masika yanamzidi kimo. Tukio la kuwapokonya askari bunduki halingeweza kutokea ila kwa muujiza, hivyo kufuta ufahamu wetu wa kimantiki. Inaeleweka mtunzi anataka kusawiri mhusika wa kike anayeonyesha ari ya kutaka kujikomboa, lakini wakati huo huo, maoni yake hayaaminiki inapogundulika matendo ya Masika yamezidi uwezo wake. Ingawa mtunzi anataka kuonyesha kupitia uwezo usio wa kawaida wa Masika kuwa, kwa vyovyote vile, udhalimu na uovu wote dhidi ya binadamu unaweza kuangamizwa; hata hivyo, uwezo huu umetiwa chumvi mno.

Vilevile, matukio ya kuachiliwa kwa Mzee Jaku kutoka jela na kupigwa risasi kwa watoto wake ni jambo lisilokubalika kisanaa kama Perinne (1978: 49) anavyodokeza kuwa "jambo litukialo kulingana na jingine kwa nasibu laweza kwa haki kutumiwa kutanguliza hadithi, na wakati mwingine kusababisha utata, lakini sio kulimaliza" (uk.4). Matukio haya yanapotukia kwa wakati mmoja

hayazami akilini kabisa. Ijapokuwa azma ya mtunzi ilikuwa ni kutuonyesha uovu uliosakini kisiwani Unguja, au tangu Jaku kutiwa mbaroni na kuachiliwa, hakuna lolote lililokuwa limebadilika, lakini, kisanaa, hatutarajii mtunzi aimalize hadithi yake kinasibu kama Perrine anavyosisitiza. Mohamed kwa njia moja au nyingine, anaonekana kuhitimisha riwaya zake ama kwa ndoa au kuwaua wahusika wakuu. Forster (1927) anawaorodhesha watunzi walio na tabia ya kuwaangamiza wahusika wakuu, au kuwaoza kuwa waandishi wastani. Akifafanua swala hili anasema “kama haingekuwa kifo na ndoa sijui ni kwa njia gani mwandishi wa riwaya wa kawaida angehitimisha riwaya yake” (uk.94).

Matukio haya yanamlazimu mhakiki kutumia kigezo cha Forster kumweka Said Ahmed Mohamed katika kundi la waandishi wastani. Hii ni kwa sababu takribani riwaya zake tangulizi, hususan *Asali Chungu* (1977), ameishia kuwaua wahusika wake wakuu:  Zuberi, Amina na Biti Daudi, ingawa kuna sababu ya kufanya hivyo— kutokomeza uchafu wa awali wa kibwanyenye na ujenzi wa jamii mpya. Tofauti na riwaya nyingine, mwandishi anahitimisha *Utengano* (1980) kwa ndoa baina ya Maimuna na Kabi. Riwaya zake zote za baadaye, kwa mfano *Kiza Katika* (1988) anaimaliza kwa kuangamiza wahusika wakuu: Mvita, Juba na Kudura. Anahitimisha riwaya ya *Tata za Asumini* (1990) kwa kumuua Asumini, ambaye ndiye mhusika mkuu. Hata hivyo, kuhitimisha riwaya zake kwa kuwaua baadhi ya wahusika isikadiriwe kama udhaifu (Forster, 1927) kwani inafahamika wazi kuwa anaongozwa na itikadi ya Kimarx anapoandika kazi zake za kubuni. Hivyo, kwa kuwaangamiza wahusika wake wakuu anataka kudhihirisha kuwa, kwa vyovyote vile, lazima maovu yaangamizwe, mapinduzi yatokee na kizazi kipya kizaliwe ili kiweze kujenga jamii isiyo doa wala toa. Pia, vifo vya wahusika hawa ni changamoto kwa wale wanaosalia katika kuendeleza vita vya ukombozi.

Muwala wa riwaya hii unaendelea kufifia kwani Mohamed hatoi uvumbuzi wa muuaji wa Bwana Hamoud kwa sababu ni wazi hakuwa Mzee Jaku. Haya yanajulikana kupitia kupitia maelezo yake kuwa “Farouk alikusanya ushahidi wa kutosha dhidi yake. Akamtumbukiza hatiani akijua bwana huyo hana hatia.” (uk. 76). Kulingana na maoni ya Forster (1927:88), “mjenzi wa msuko anatarajia, kama wasomaji, tukumbuke, nasi tunamtarajia asiache masuala yanayoning’inia ...” (uk.88). Hivyo, katika mkabala huu, Said Ahmed Mohamed aliwajibika kututegulia kitendawili cha muuaji wa babake Fauz— Hamoud. Ni kutokana na haya ambapo kidole cha lawama kinamlenga mtunzi kwa kutofuma matukio kwa uzi mmoja. Hali hii inadhihirisha mkatiko katika msuko mzima wa riwaya hii.

Waaidha, baadhi ya makosa yanayosababishwa na kutoumana kwa baadhi ya matukio na wahusika katika msuko wa riwaya hii yanapoibuliwa, haimaanishi haina uzuri wowote au mtunzi anaonewa. Hili ni jambo ambalo Mohamed (1981: 9), hata yeye mwenyewe, amelikubali katika makala ya “Kupatana na Riwaya Zangu” anaposema:

> Lakini ninaposoma *Asali Chungu* au *Utengano* sasa, huuma kidole nikijuta makosa niliyoyafanya ambayo ningaliweza kuyaepuka. **Si kama *Dunia Mti Mkavu* haina makosa, lakini hayo machache yaliyomo ni machache zaidi hasa katika kipengele cha ploti** ikilinganishwa na viwili vilivyotangulia. (*Msisitizo ni wa mwandishi wa makala.*)

Kulingana na mtunzi mwenyewe, riwaya yake ina baadhi ya makosa ambayo yanaudhoofisha muwala wake baina ya matukio na vitendo vya wahusika. Mwishoni mwa riwaya inadhihirika uhusiano wa matukio na vitendo vya wahusika kwa ujumla unakosekana. Kwa hali hii, mwandishi wa makala hii anakubaliana na Hawkes (1977), anaposema kuwa "... hali halisi ya vitu sio katika vitu vyenyewe, bali ni mahusiano ambayo tunajenga baina ya vitu husika" (uk.17). Kulingana na maoni ya Hawkes (1977), lazima mahusiano yaliyopo baina ya vitu yatiliwe maanani, ila sio katika vitu vyenyewe.

Uhusiano wa msuko na vitendo vya wahusika vinapochunguzwa, mwishoni mwa riwaya ya *Dunia Mti Mkavu*, ni dhahiri uhusiano huu unakosekana, jambo ambalo linaifanya kukosa muwala. Kwa hali hii, Antico na Hazelrigg (1970), wakigusia juu ya uhusiano wa msuko na matendo ya wahusika wanasema, "... msuko wa riwaya unafafanua matendo ya wahusika, hivyo hutusaidia kuelewa hulka za wahusika" (uk.348). Kulingana na mawazo ya waandishi hawa, msuko hufafanua vitendo vya wahusika. Ni kutokana na maoni haya ambapo uamuzi unafikiwa kuwa, ikiwa vitendo vya wahusika havioani na matukio katika msuko, muwala katika riwaya nzima unakosekana, hivyo kukosa ukamilifu na utimilifu wa kifasihi kwa kiwango fulani.

## Muwala wa msuko, wahusika, mandhari na mtindo katika *Kiza Katika Nuru* (1988)

Katika sehemu inayotangulia, muwala wa vipengele vya fani katika *Dunia Mti Mkavu* (1980) umejadiliwa ili kufikia maamuzi iwapo riwaya husika imefikia ukamilifu na utimilifu wa kifasihi. Katika sehemu hii, pia, vipengele hivi vinachunguzwa vinavyoumana ili kuukamilisha muundo wa riwaya ya *Kiza Katika Nuru*, hivyo kuleta maana kamili na kuweza kufikia ukamilifu na utimilifu wa kifasihi. Kimsingi, vipengele hivi haviwezi kutenganishwa iwapo ukadiriaji wa ufaulu kwa mtunzi unahitajika kama James (1975: 44) anavyosema kuwa:

> riwaya ni kama kiumbe kilicho na uhai, chenye umoja; na kama kinavyoendelea na kuishi inagundulikana kuwa … katika kila sehemu kuna uhusiano wa aina fulani katika sehemu zile zingine.

Kulingana na maoni ya James, kila sehemu ya riwaya, iwe ni msuko, wahusika au mandhari huwa na uhusiano na sehemu zile zingine.

Riwaya ya *Kiza Katika Nuru* inapochunguzwa kwa makini; inaibuka kuwa matendo ya wahusika yanaenda sambamba na mandhari na matukio mbalimbali

yanayotendeka katika riwaya nzima. Mvita anapoingia ofisini mwa babake Juba, anaikagua kama ndio mara ya kwanza kuiingia. Mvita na babake wanaonekana kuwa katika mazingira yenye baridi nyingi: "Fani ubavuni pake linazunguka kuzidisha baridi katika baridi ya 'air condition' inayonguruma. Ile baridi ya 'air condition' ingetosha kumtetemesha Mvita" (uk. 12). Mandhari haya yanaashiria uhusiano mbaya uliopo baina ya mwana na babake. Uhusiano wao ni baridi kama chumba chenyewe. Mazingira yanayomzunguka Mvita yanamfanya kuwa mgumu katika fikra zake anapozungumza na babake. Yuko tayari kuasi tabaka la babake na kujiunga na tabaka la wachochole. Vivyo hivyo, tabia ya Juba inadhihirika waziwazi kupitia mandhari ya ofisi yake. Anajifanya mambo yako shwari, ndiposa hahisi baridi inayotawala chumba chake. Kama mwanaye, msimamo wake ni mkali; hayuko tayari kubadilisha uraibu wake wa kulimbikiza mali. Hivyo, kwa sababu ya kutofautiana kimawazo, mtunzi anawaweka katika mazingira yanayodhihirisha uhusiano mbaya uliopo baina ya baba na mwanaye. Aidha, kibonzo cha nyoka anayemfukuza chura, huku chura akimfukuza kurumbiza ukutani mwa Juba, kinadhihirisha uhusiano uliopo baina ya maskini na matajiri; mafukara wakiongozwa na Mvita na wakwasi wakiongozwa na Juba. Moja kwa moja, uhusiano uliopo baina ya mandhari, wahusika, msuko na mtindo wa mtunzi kupitia kibonzo kinachoiremba ofisi ya Bwan Juba unadhihirika. Kibonzo hiki, ambacho ni sehemu ya mandhari, bila shaka, kupitia jazanda za chura na nyoka; huku chura akiashiria Mvita, naye nyoka akiwakilisha Bwan Juba.

Tabia za wahusika hawa zinadhihirika katika jazanda hii. Chura katika hali ya kawaida hafui dafu mbele ya nyoka; hali yake ni ya unyonge, lakini mara tu anapochokozwa na hana lingine la kufanya, hubadilika na kumwinda nyoka. Hivi ndivyo inavyodhihirika katika hulka za Mvita. Ingawa anamheshimu na kumwogopa babake, wakati umefika wa kumuasi, ndiposa mandhari inayowazunguka imetawaliwa na baridi tupu– "baridi katika baridi ya 'air condition' (uk. 12). Jazanda ya nyoka inaenda sambamba na hulka za Juba. Katika hali ya kawaida, nyoka ni mkaidi na kila mara anamwinda chura. Hii ndio sababu Juba anapozungumza na Mvita na kuasi mipango yake, anamfukuza kazini na nyumbani, huku akimuahidi kumwangamiza: "Maadamu unanielekeza sindano Mvita, mimi nitakuelekeza mtaimbo" (uk. 25). "Sindano" inamaanisha madogo Mvita anayomtendea babake hali "mtaimbo" ni kifo kilichomkabili Mvita baadaye. Lugha ya vitisho anayoitumia Juba ina ufungamano mkubwa na hulka zake. Ukatili wake haufichiki, kwani baadaye, anamuelekeza mtaimbo aliomuahidi, kwani anamuua kupitia Shanzia (aliyekuwa rafiki ya Mvita na waliosoma pamoja.)

Halikadhalika, moja kwa moja, inaeleweka kupitia jazanda anazozitumia Juba kutoa onyo kwa Mvita zinageuka kuwa kiungo muhimu cha matukio ya baadaye, yaani, kifo cha Mvita kinapotekelezwa kwa ukatili mkubwa na Shazia

na genge lake. Ni kutokana na haya ambapo muwala na uhusiano uliopo kati ya mandhari, matendo ya wahusika na vipengele vya mtindo anavyovitumia mtunzi unadhihirika. Kwa hali hii, maoni ya Antico na Hazelrigg (1970: 359) yanawafiki haya wanaposema kuwa:

> Maneno anayoyachagua mtunzi na jinsi anavyoyapanga ni sehemu ya wahusika na mandhari. Kipengele hiki cha ubunifu hakiwezi kutenganishwa na vile vingine vitatu kwani ni kupitia maneno, tukio, mhusika na mandhari vinaweza kuelezwa kwa msomaji.

Maoni ya wataalamu hawa yanafafanua suala hili, bila kubakisha, kwani mandhari ambayo mtunzi anawajengea Mvita na Juba yanafanana na hulka zao wakati huo. Lugha anayotumia Juba yenye kuashiria mabaya kwa Mvita haikosi kuhisika na kuona jinsi inavyoshaajishwa na mazingira mabaya yanayomzunguka Juba. Waaidha, tunashuhudia migogoro mingine inayofuata katika riwaya nzima. Vilevile, kutokana na mandhari ya kimaskini yanayomzunguka Mvita, yanamshajiisha kuanza kupigania usawa kwa wote. Ni kutokana na mabadiliko haya ambapo mgogoro baina ya Mvita na babake unashuhudiwa. Uhusiano mkavu baina yao unadhihirika kupitia baridi inayotamalaki ofisi ya Juba. Juba anayezungukwa na mandhari ya kikwasi, yuko tayari kupigana kwa kila njia kudumisha hali hii. Kwa upande mwingine, hali hii ya kikwasi ndiyo inayopingwa na Mvita; jambo ambalo linamfanya kuanzisha mahubiri ya kuwatoa wachochole kizani hadi nuruni. Kutokana na mchuano wa Juba na Mvita, migogoro kadhaa inajitokeza na kuusukuma mbele msuko wa riwaya hii. Forster (1927), akionyesha muwala na uhusiano wa matukio na wahusika anasema “Matukio hutokana na wahusika, na matukio haya yakiwa yametendeka humbadilisha mhusika. Wahusika na matukio yana uhusiano wa karibu sana … (uk. 90). Tunapotathmini dondoo hii, tunafahamu kuwa ni vigumu kutenganisha msuko na wahusika kwani wahusika huzua matukio na matukio yayo hayo humbadilisha mhusika.

Katika *Kiza Katika Nuru*, muwala uliopo baina ya matukio na matendo ya wahusika unajitokeza waziwazi. Mzozano baina ya Mvita na Juba unadhihirisha mgogoro unaowakilisha jamii pana. Juba anapowafukuza Mvita na mamake Kudura kutoka nyumbani, uhusiano mbaya uliopo baina ya wahusika hawa unafahamika moja kwa moja. Ni kutokana na tukio hili la Mvita na Kudura kufukuzwa nyumbani ambapo unyama wa Juba unaeleweka. Hana shukrani kwa mkewe kwa sababu anasahau jinsi alivyomsaidia kukwea na kufikia mlima wa utukufu wa kiuchumi na kisiasa; anageuka kuwa punda ambaye asante yake ni mateke na mashuzi. Kufukuzwa kwao kunageuka kuwa kisasi na kunawashajiisha kuendeleza mapambano ya ukombozi dhidi ya tabaka linalowanyanyasa. Ari na juhudi zao, zinashuhudiwa mtunzi anapowapitisha kwenye kiza totoro wanapoenda kuonana na wazee wa kijiji cha Maweni. Ingawa wanapitia kwenye kiza totoro hawaonyeshi woga wowote. Kiza kinachowazunguka Mvita, Kudura

na Simbamwene kinadhihirisha ukakamavu na ujasiri wao katika kupigania haki zao. Mandhari yanayowazunguka wahusika hawa yana ufungamano mkubwa na hulka zao; yanadhihirisha juhudi zao za mapambano. Kwa vyovyote vile, hawako tayari kurudi nyuma.

Zaidi ya kuwaweka katika mandhari ya kuogofya, mtunzi anawaingiza Mvita na Kudura baharini ili wachote mchanga mweupe. Anapowaweka katika mazingira ya aina hii, anataka kutudhihirishia ugumu uliopo katika mapambano ya ukombozi. Mchanga mweupe wanaouchota baharini ni ishara ya utakaso na ujenzi wa jamii mpya isiyo na doa wala toa. Mwandishi hangewajengea mazingira tofauti, kwani kama wapigania ukombozi, lazima wapitie katika majaribu mengi na magumu. Ni wazi jinsi mandhari haya yanavyoenda sambamba na matendo ya wahusika. Hivyo, kuona muwala uliopo baina ya mandhari, vitendo vya wahusika na matukio yanayosababishwa na wahusika hawa; matukio ambayo ni muhimu katika kuendeleza msuko wa riwaya nzima hadi kufikia upeo wake. Mgogoro wa kinafsia unaopita akilini mwa Mvita wanapopita na kuzungukwa na kiza kisicho na matumaini wanapoenda kukutana na wazee wa Maweni unadhihirika (uk. 181). Hata hivyo, katika kiza hiki anaona kuna alama ya nuru. Nuru hii katika nafsi yake inampa matumaini mapya katika mapambano ya ukombozi wa kijamii na kiuchumi.

Fauka ya haya, kutokana na mandhari ya kiza na nuru anayowajengea Mvita, Kudura na Simbamwene, pia, ufungamano uliopo baina ya wahusika na ishara za kiza na nuru unapambanuka. Kiza, huku kikienda sambamba na matendo mabaya yanayotendwa na watu kama Juba hali nuru ikisimama kama mnara wa mema. Ishara hizi ndizo zinazojenga kiini cha riwaya nzima. Mvita yuko katika harakati za kutafuta nuru, huku akijibidiisha kuondoa kiza. Mvita ameazimia kuubadilisha mfumo wa kibepari unaoongozwa na babake Juba ili kuleta usawa kwa wote. Hivyo, kipengele cha mandhari (ya kiza na nuru), kinapounganishwa na hulka za Mvita na Kudura na mtindo kupitia ishara za kiza na nuru, inafahamika wazi kiini cha riwaya nzima. Kuhusiana na jambo hili Antico na Hazelrigg (1970: 346) hawachelei kusema kuwa:

> Ni kupitia muungano wa vipengele vinne vya kimsingi vya kazi ya ubunifu, ambapo maudhui huibuka. Pia, kuelewa maana ya vipengele hivi ni muhimu ili kufikia uamuzi wa mwisho kuhusu muundo wa kazi ya fasihi.

Katika hali hii, ufungamano uliopo baina ya mandhari, msuko, vitendo vya wahusika na mtindo unadhihirika; ufungamano ambao unaibua maudhui ya riwaya nzima. Hivyo, tunafahamu utegemeano na uhusiano uliopo baina ya vipengele hivi. Mandhari yanapambanua vitendo vya wahusika, hali vitendo hivi vinazua migogoro ambayo inaifikisha riwaya husika katika kilele chake. Hawkes (1977: 18), akigusia mahusiano ya vipengele mbalimbali vya tungo anasema:

> Kwa wanaumuundo, hali ya kila kipengele katika kila muktadha hakina umuhimu kibinafsi na katika hali ya kawaida, huongozwa na uhusiano wa vipengele vingine vinavyohusika katika muktadha huo.

Kulingana na Hawkes (1977), umuhimu wa kila kipengele unatokana na uhusiano wa kipengele husika na vile vingine. Hivyo, katika *Kiza Katika Nuru*, mtunzi anapanga vipengele mbalimbali vikidhihirisha muwala na uhusiano, huku vikionyesha kutegemeana.

Mbali na haya, mandhari yanayomzunguka Kudura, yanapochunguzwa inafahamika yanadhihirisha ukakamavu, uvumilivu na uzoefu wa maisha magumu. Kutoka mwanzo wa riwaya tunakumbana na mazingira ya kilitima yanayomzunguka hali ambayo inamshajiisha kuwa mvumilivu na mwenye moyo imara. Katika kumbukumbu za baadhi ya mandhari ya kinobe msanii anayomjengea fakiri wake anasema, "Alivuta [Kudura] kiwi cha mlango-mbao zake zilizokongoka, bawaba zilimfuata pasi na kizuizi, zikagonga ukuta. Mtapanyiko wa nzi waliokuwa waking'ong'a uani ulistushwa na mgongo wa mlango na kile kikundi cha nzi kilichotapia kuingia ndani kilimvaa na kutapakaa" (uk. 48). Mazingira ya aina hii ndiyo yanakamilisha sehemu ya maisha ya Kudura. Hata hivyo, anavumilia vituko vya Bwan Juba na kuwa mtiifu. Ndiposa wimbo wa "Mwana Kupona" uliokuwa ukiimbwa na marehemu mamake Mosi, unamfundisha kukaa na bwanaye Juba hata ikiwa ndoa yao imejaa mazonge matupu. Wimbo huu, ambao unajitokeza kama kipengee cha mtindo, unaibuka kuwa muhimu katika kuchangia na kudhalilisha tabia ya Kudura. Unamfanya mnyenyekefu na mtiifu kijinga kwa Juba. Hajiulizi kwa nini, kwa vipi na kwa sababu gani mambo yatendeke, hata baada ya ushawishi wa wanawe wawili: Mvita na Mbishi. Vilevile, wimbo huu unageuka kuwa kiungo cha matukio yanayomuathiri Kudura– ushawishi wa Mvita na Mbishi ili aasi vituko vya Juba, baba yao. Kumfanya Kudura ajikute katika mazingira ya mkwaruzano baina ya Bi. Patima na Asuman, mumewe, na vituko vya Biti Jabu na muuza nyama, yamepangwa kimakusudi ili kumtayarisha kumbadilisha kitabia. Kutokana na mazingira haya tunaambiwa:

> Taratibu majilio mapya yalijiiba kwenye nafsi ya Kudura. Kila siku ilikuwa mpya. Kila siku ilikuwa tofauti na nyingine, jana si leo na leo si kesho. Maswali adimu yalijiri kwake, 'kwa nini?' Alijiuliza, 'kwa sababu gani?' na tena 'vipi? Ilikuwaje? Ikendaje?' Taratibu aliyatia mambo yote katika mizani: kupanda na kushuka, mkanganyo ukakanganyuka. Likabaki lililobaki akilini mwake. Picha ya yeye alivyo, maafa yake, shida zake, unyonge wake na sababu ya yote haya: Nani adui yake hasa? Ndiye au siye? Hatimaye kweli ilipodhihiri, salio la yote hayo ilikuwa Bwan Juba' (uk.128-129).

Dondoo hii inafafanua chanzo cha mabadiliko ya Kudura. Ni kutokana na mandhari yenye vituko ambapo Kudura anazaliwa upya; kutoka Kudura mpole, mstahimilifu, mtiifu, mpole, mjinga na limbukeni, na kuchukua jina la ubatizo: Kudura simba jike, mkali, mtetezi wa haki, mwerevu na mtaka kumparura mumewe kwa pauro. Uwasilishaji dhahiri na mazungumzo ya Kudura yasiyohitaji majibu anapomzomea Juba, mumewe, kunadhihirisha ukali alionao. Ukali huu haungehisika na mabadiliko ya Kudura kitabia haungedhihirika kama mtunzi angetumia mbinu nyingine ya uwasilishaji, hususan uzungumzi nafsia au mazungumzo ya moja kwa moja baina ya wahusika. Mgogoro baina ya mkemtu na mumemtu ndio unamsukuma Kudura hadi mashambani na kuanzisha maisha mapya. Anashirikiana, bega kwa bega, na Mvita, mwanaye, kupambana na udhalimu wa tabaka dhalimu. Mgogoro huu unazaa matunda kwani watu wa kijiji cha maweni wanawapokea kwa mikono miwili. Kufikia hapa, mandhari yanayojengewa Kudura, yanaenda sambamba na mabadiliko ya tabia zake, na yanamhamasisha kuitikia vilivyo. Yanamshajiisha na kumchochea kupigania haki yake na wanawake wote kwa ujumla.

Sio tu muwala wa msuko, mandhari na uumbaji wa wahusika, unaojitokeza, bali pia, muumano wa mtindo na msuko wa riwaya nzima ni bayana. Kuanzia mwanzo wa riwaya hadi mwisho, mtunzi anatumia viangaza mbele vinavyobashiri hatima ya mhusika mkuu Mvita, na wakati huohuo, vinafuma kwa pamoja matukio mbalimbali katika msuko mzima. Mwanzoni mwa riwaya hadi mwisho, mtunzi anatumia viangaza mbele vinavyobashiri hatima ya mhusika Mvita. Mwanzoni mwa riwaya, tunashuhudia ndoto ya Kudura (uk. 44) ambayo inajitokeza kama kiangaza mbele, huku kikibashiri hatari inayomkabili Mvita. Pia, kupitia ndoto hii uhusiano wa Mvita na Juba, babake, ambaye yuko tayari kumwangamiza unajitokeza. Bundi wanaotoa vilio (uk. 180) huku wakipokezana na Komba, vilevile, wanabashiri mabaya ambayo yangemfika Mvita baada ya kuonana na wanakijiji wa Maweni. Kwa kweli, baadaye anaangamizwa na babake wa kumzaa, Juba kupitia Shanzia na genge lake. Hata hivyo, kiangaza mbele kinachojitokeza kama vita baina ya kaa mdogo na mkubwa (uk. 194), tunatolewa ishara ya mafanikio katika harakati za Mvita za kutaka kuubadilisha mfumo unaotweza na kumdhalilisha mnyonge. Ingawa Mvita anaangamizwa na Shanzia kupitia mpango wa Juba, kuna matumaini makubwa katika mimba ya Salma ambayo inasimama kama ishara ya kizazi cha kesho ambacho kingeendeleza mapambano ya ukombozi na hatimaye, ujenzi wa jamii mpya kufuata.

Vivyo hivyo, mtunzi anatumia viangaza mbele katika kufuma matukio ya riwaya yake kwa kutubashiria sherehe za kifo cha Mvita kupitia kunguru (uk. 193) wanaosheherekea matumbo ya samaki, huku paka wakijisopeka katika sherehe bila kualikwa, na kuchukua sehemu ya matumbo haya kwa nguvu. Baadaye paka hawa wanageuka kuwa Mbishi na Kudura, mamake, ambao wanajisopeka katika sherehe za kusheherekea kifo cha Mvita na kumuua Juba

kwa ukatili mkubwa ili kulipiza kisasi. Moja kwa moja, ufungamano uliopo baina ya viangaza mbele anavyovitumia mwandishi na maisha ya wahusika, hususan Mvita, Juba, Kudura na Mbishi unadhihirika. Bila shaka, kupitia viangaza mbele ambavyo ni vipengele vya kimtindo, muwala uliopo baina ya msuko, mandhari na wahusika katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru* unajitokeza. Hivyo, muwala na uhusiano wa vipengele hivi unadhihirika katika kilele cha ujumbe wa mtunzi wa kupigania ujenzi wa jamii mpya; ambao pasipo mapambano hauwezi kupatikana.

Hadi sasa, inadhihirika wazi kuwa Said Ahmed Mohamed amefuzu katika kuunda vipengele vya fani vinavyoumana na kuhusiana ili kukamilisha muundo wa riwaya hii na kuifikisha katika kilele cha ukamilifu na utimilifu wa kifasihi kwa kiwango kikubwa. Kwa vyovyote vile, muwala wa vipengele vya fani katika riwaya zote mbili unapolinganishwa, inadhihirika kuwa Mohamed amefaulu zaidi katika riwaya ya *Kiza Katika Nuru* kuliko *Dunia Mti Mkavu* kifani. Ingawa Mazrui (1982) anaiona riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* kuwa maarufu kimaudhui, hata hivyo, *Kiza Katika Nuru* inafaulu kwa kiwango kikubwa kifani.

## Hitimisho

Uhakiki wa riwaya mbili za Said Ahmed Mohamed umeonyesha misuko inayodhihirisha uchangamano, na hasa msuko wa *Dunia Mti Mkavu.* Hata hivyo, msuko wa riwaya hii umeonyesha mkatiko wa matukio kiwakati; jambo ambalo unaidhoofisha. Riwaya ya *Kiza Katika Nuru*, inadhihirisha muwala na mzuano wa matukio mbalimbali, hivyo kuwa na mshikamano. Vilevile, msuko wa *Dunia Mti Mkavu*, unaonyesha kubuniwa katika misingi ya Fasihi Simulizi ya Kiafrika ambapo vijihadithi mbalimbali vinawakilisha matukio tofauti. Kila kijihadithi kinaendelezwa na mhusika mkuu, pamoja na wahusika wasaidizi.

Riwaya ya *Dunia Mti Mkavu* ni mojawapo ya riwaya za Said Ahmed Mohamed zenye msuko changamano. Uchangamano huu umetingwa na matatizo ya mkatiko wa uwasilishaji wa baadhi ya matukio. Hivyo basi, mkatiko huu wa matukio unaathiri muwala wa uumbaji wa wahusika na ujenzi wa msuko mzima. Ni kutokana na ukosefu huu wa muwala baina ya wahusika na msuko, ambapo inadhihirika kuwa umaarufu wa riwaya hii unaodokezwa na Mazrui (1982) kwa upande wa maudhui unafifia kwa upande wa fani na kuikosesha ukamilifu na utimilifu wa kifasihi kwa kiwango fulani. Hii ni kwa sababu riwaya bora ni ile inayodhihirisha umaarufu kwa upande wa maudhui na fani. Aidha, riwaya ya *Kiza Katika Nuru* inaonyesha umaarufu zaidi kwani vipengele vyote vya fani vinadhihirisha muwala, hali ambayo inaifanya kufikia ukamilifu na utimilifu wa kifasihi wa maandishi ya kubuni kwa kiwango kikubwa.

## Marejeleo


Antico, I., & Hazel, M. K. (1970). *Insight Through Fiction: Dealing With the Short Story.* Melopark, California: Gummzug Publishing Company, Inc.

Barthes, R. (1966). An Introduction to the Structuralist Analysis of Narratives. In C. Kaplan (Ed.), *Criticisms: The Major Statements.* New York: St.Martins Press, Inc.

Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction.* Minneapolis: University of Minnesota Press.

Forster, E. M. (1927). *Aspects of the Novel.* Harmoundsworth: Penguin Books.

Hawkes, T. (1977). *Structuralism and Semiotics.* London: Methuen.

James, H. (1961). The Art of Fiction. In Scholes Robert (Ed.), *Approach to the Novel: Materials for Poetics.* San Francisco: Chandler Publishing Company.

Jessee, M. J., Wafula, R. M., & King'ei, K. G. (2018). Uhusiano wa Itikadi na Mtazamo wa Mtunzi: Uchunguzi wa Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed. Katika Omari, S. na Samwel, M. (Wahariri), *Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika: Kwa Heshima ya Prof. M. M. Mulokozi.* Dar es Salaam: TATAKI.

Kimmey, J. L. (1976). *Experience and Expressions: Reading and Responding to Short Fiction.* Illinois: Scott Foresman.

Kiiru, D. H. (1987). Theory of Literature: An Introduction to Literary Criticism. Seminar Paper, Nairobi: University of Nairobi.

Levi-Strass, C. (1967). *Structural Anthropology.* Gargen City: Anchor Books.

Mazrui, A. (1984). Dunia Mti Mkavu: A Swahili Literary Treatise on Marxism. *KISWAHILI.* Juzuu la 51/1. DSM: Chuo Kikuu Cha Dar e salaam.

Mohamed, S. A. (1980). *Dunia Mti Mkavu.* Nairobi: Longman.

_____________ (1981). Kupatana na Riwaya Zangu. *MWAMKO: Jarida la Chama cha Kiswahili.* Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

_____________ (1988). *Kiza Katika Nuru.* Nairobi : Oxford University Press.

Ngara, E. A. (1982). *Stylistic Criticism and the African Novel.* London: Heinemann Educational Books.

Newton, K. M. (1988). *Twentieth Century Literary Theory.* New Hampshire: Macmillan Press Ltd.

Perrine, L. (1978). *Literature: Structure, Sound and Sense* (3rd Edition). New York: Harcourt Brace Javanovich, Inc.

Scholes, R. (1974). *Structuralism in Literature: An Introduction*. New Haven: Yale University Press.

Warren, A. (1961). Nature and Modes of Fiction. In R. Scholes (Ed.). *Approaches to the Novel: Materials for a Poetics.* San Francisco: Chandler Publishing Company.